جمعية خدمة المحتوى الإسلامي باللغات
ضيوف الرحمن
hajjumrh.com



Dua kutoka katika

Qur'ani na Sunna

Kiswahili

سواحيلي

ضيوف الرحمن
hajjumrh.com

Partners in Implementation

Content Association
Rowad Translation
Byenah
IslamHouse

This publication may be printed and disseminated by any means provided that the source is mentioned and no change is made to the text.

Tel : +966 50 244 7000
info@islamiccontent.org
Riyadh 13245-2836
www.islamiccontent.org

Dua kutoka katika Qur'ani na Sunna

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu peke yake, na rehema na amani ziwe juu ya yule ambaye hakuna nabii baada yake.



1. Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa kurehemu
2. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote
3. Mwingi wa rehema, Mwingi wa kurehemu
4. Mmiliki wa siku ya Malipo
5. Ni wewe peke yako tunayekuabudu na ni wewe peke yako tunayekutaka msaada
6. Tuongoe njia iliyonyooka
7. Njia ya wale uliowaneemesha. Siyo ya wale waliokasirikiwa, wala waliopotea. Suratul- Faatiha: 1-7
8. Ewe Mola wetu Mlezi! Tukubalie! Hakika Wewe ndiye Msikivu, Mwenye kujua yote. Suratul-Baqarah: 127

8 Ewe Mola wetu Mlezi! Tukubalie! Hakika Wewe ndiye Msikivu, Mwenye kujua yote. Suratul-Baqarah: 127



9 Na tusamehe makosa yetu, hakika Wewe ni mwenye kukubali zaidi msamaha, Mwingi wa kurehemu. Suratul-Baqarah: 128

10 Ewe Mola wetu Mlezi, tupe duniani mema na akhera tupe mema na utukinge kutokana na adhabu ya Moto. Suratul-Baqarah: 201

11 Tumesikia na tumetii. Tunakutaka maghufira Mola wetu Mlezi! Na marejeo ni kwako. Suratul Baqara: 285

12 Mola wetu Mlezi! Usituchukulie ubaya tukisahau au tukikosea. Mola wetu Mlezi! Usitubebeshe mzigo kama uliyowabebesha wale waliokuwa kabla yetu. Mola wetu Mlezi! Usitutwike tusiyoyaweza, na uyatupilie mbali mabaya yetu, na utusamehe na uturehemu. Wewe ndiwe Mlinzi wetu. Basi tupe ushindi dhidi ya kaumu ya makafiri. Suratul Baqara: 286

13 Mola wetu Mlezi! Usizipotoe nyoyo zetu baada ya kutuongoa, na tutunuku rehema itokayo kwako. Hakika, Wewe ndiwe Mwenye kutunuku mno." Surat Al Imraan: 8

14 "Mola wetu Mlezi! Hakika, sisi tumeamini. Basi tusamehe dhambi zetu, na tuepushe na adhabu ya Moto." Surat Al-Imran: 16

15 "Mola wangu Mlezi! Nitunuku kutoka kwako dhuria (kizazi) chema. Hakika, Wewe ndiye unayesikia maombi." Surat Al-Imran: 38

16 "Mola wetu Mlezi! Tuliyaamini uliyoyateremsha, na tulimfuata Mtume huyu, basi tuandike pamoja na wanaoshuhudia." Surat Al-Imran: 53



17 "Mola wetu Mlezi! Tufutie dhambi zetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu, na isimamishe imara miguu yetu na utunusuru dhidi ya kaumu ya makafiri." Surat Al-Imran: 147

18 "Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Sub-haanaka (umetakasika)! Basi tukinge kutokana na adhabu ya Moto.

19 Mola wetu Mlezi! Hakika, yule unayemuingiza Motoni, basi umemhizi (umemfedhehesha). Na waliodhulumu hawana wasaidizi wowote.

20 Mola wetu Mlezi! Hakika, sisi tumemsikia muitaji akiita kwenye Imani kwamba: Muaminini Mola wenu Mlezi; kwa hivyo, tukaamini. Basi tufutie dhambi zetu, na utufunikie makosa yetu, na utufishe pamoja na walio wema.

21 Mola wetu Mlezi! Na utupe yale uliyotuahidi kwa Mitume wako, wala usituhizi (usitufedheheshe) Siku ya Kiyama. Hakika, Wewe huvunji miadi."Surat Al Imraan: 191-194

22 "Mola wetu Mlezi! Tuliamini, basi tuandike pamoja na wanaoshuhudia." Surat Al-Maaidah: 83

23 "Mola wetu Mlezi! Tumezidhulumu nafsi zetu, na kama hutatufutia dhambi na ukaturehemu, hakika tutakuwa katika waliohasirika." Suratul A'araaf: 23

24 "Mola wetu Mlezi! Usitujaalie kuwa pamoja na kaumu madhalimu." Suratul A'araaf: 47



25 **Ewe Mwenyezi Mungu,** "Wewe ndiye rafiki mlinzi wetu. Basi tusitiri dhambi na uturehemu. Na Wewe ndiwe Mbora zaidi wa wasitirio dhambi. Na utuandikie mema katika dunia hii na katika Akhera." Suratul A'araaf: 155-156


26 "Mwenyezi Mungu ananitosha. Hakuna mungu isipokuwa Yeye tu. Mimi ninamtegemea Yeye, na Yeye ndiye Mola Mlezi wa Kiti Kikuu cha Enzi." Surat At-Taubah: 129

27 "Mola wetu Mlezi! Usitufanye wenye kutiwa majaribio na hao kaumu madhalimu.

28 Na utuokoe kwa rehema yako kutokana na kaumu hawa makafiri." Surat Yuunus: 85-86

29 "Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ninajikinga kwako kutokukuomba nisilo na elimu nalo. Na kama hunisamehe na kunirehemu, nitakuwa katika waliopata hasara." Surat Hud: 47

30 **Ewe Mwenyezi Mungu, ewe** "Muumba wa mbingu na ardhi! Wewe ndiye Mlinzi wangu katika dunia na Akhera. Nifishe hali ya kuwa ni Muislamu na niunganishe na walio wema." [Surat Yusuf: 101][1] .



1- Angalia kwa ajili ya faida: Kitabu Al-Fawaaidi cha Ibn Qayyimi, Ukurasa wa 436-437.

31 "Ewe Mola wangu Mlezi! Ujalie mji huu uwe wa amani, na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu." Surat Ibrahim: 35

32 "Mola wangu Mlezi! Nijalie niwe mwenye kusimamisha Swala, na katika dhuria yangu pia. Ewe Mola wetu Mlezi, na ipokee dua yangu." Surat Ibrahim: 40

33 "Mola wetu Mlezi! Nighufirie mimi na wazazi wangu wote wawili, na Waumini, siku itakaposimama hesabu." Surat Ibrahim: 41

34 "Ewe Mola wangu Mlezi! Nikunjulie kifua changu.

35 Na nirahisishie kazi yangu hii.

36 Na lifungue fundo lililo katika ulimi wangu." Surat At-Twaha: 25-28

37 "Mola wangu Mlezi! Nizidishie elimu." Surat Twaha: 114

38 "Hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki ila Wewe, utakasifu ni wako. Hakika mimi nilikuwa katika madhalimu." Surat Al-Anbiya: 87

39 "Mola wangu Mlezi! Najikinga kwako na wasiwasi wa mashetani.

40 Na najikinga kwako, Mola wangu Mlezi, wasinikaribie." Suratul-Muuminun: 97-98

41 "Mola wetu Mlezi! Tumeamini; basi tusamehe na uturehemu, nawe ndiwe Mbora wa wanaorehemu." Suratul-Muuminun: 109





42 "Mola wangu Mlezi, Samehe na urehemu nawe ni Mbora wa wanaorehemu." Suratul-Muuminun: 118

43 "Mola wetu Mlezi! Tuondolee adhabu ya Jahannam. Hakika adhabu yake ikimpata mtu haimuachi."

44 Hakika hiyo ni kituo na makao mabaya." Surat Al-Furqaan: 65-66

45 "Mola wetu Mlezi! Tupe katika wake zetu na wana wetu yaburudishayo macho, na utujalie tuwe viongozi kwa wacha Mungu." Surat Al-Furqaan: 74

46 "Mola wangu Mlezi! Nitunuku hukumu na uniunganishe na walio wema.
Na unijalie nitajwe kwa wema na watu watakaokuja baadaye.
Na unijalie katika warithi wa Bustani za neema." Surat Ash-shu'araa: 83-85


47 "Wala usinihizi (usinifedheheshe) Siku watakapofufuliwa.

48 Siku ambayo mali haitafaa kitu wala wana.

49 Isipokuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo safi."Surat Ash-shu'araa: 87-89



50 "Ewe Mola wangu Mlezi! Nizindue niishukuru neema yako uliyonineemesha mimi na wazazi wangu, na nipate kutenda mema uyapendayo, na uniingize kwa rehema yako katika waja wako wema."Surat An-Naml: 19



51 "Mola wangu Mlezi, hakika mimi nimejidhulumu mwenyewe. Basi nisamehe." Surat Al-Qasas: 16

52 "Mola wangu Mlezi, niokoe kutokana na watu madhalimu." Surat Al-Qasas: 21

53 "Huenda Mola wangu Mlezi akaniongoa njia iliyo sawa." Surat Al-Qasas: 22

54 "Mola wangu Mlezi, hakika mimi ni mhitaji wa heri utakayoniteremshia."Surat Al-Qasas: 24

55 "Ewe Mola wangu Mlezi, ninusuru kutokana na watu waharibifu hawa!" Suratul-Ankabuut: 30

56 "Ewe Mola wangu Mlezi! Nitunuku aliye miongoni mwa watenda mema." Surat Asswaafaat: 100

57 "Mola wangu Mlezi! Niwezeshe nishukuru neema zako ulizonineemesha mimi na wazazi wangu, na nitende mema unayoyapenda. Na unitengenezee dhuria zangu. Hakika mimi nimetubu kwako, na hakika mimi ni miongoni mwa Waislamu."Suratul-Ahqaaf: 15

58

"Mola wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwa Imani, wala usijalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walioamini. Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye kurehemu mno."

Suratul-Hashr: 10

59

"Mola wetu Mlezi! Juu yako tumetegemea na kwako tunajikurubisha na kwako ndio marejeo."

Suratul-Mumtahina: 4

60

"Mola wetu Mlezi! Usitufanyie mtihani kwa waliokufuru. Na tusamehe, Mola wetu Mlezi. Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hekima." Suratul-Mumtahinah: 5

61 "Mola wangu Mlezi! Nighufirie mimi na wazazi wangu, na kila aliyeingia nyumbani mwangu akiwa ni mwenye kuamini, na Waumini wote wanaume, na Waumini wanawake." Surat Nuuh: 28

62 **"Mola wetu Mlezi! Tukamilishie nuru yetu na utusamehe. Hakika Wewe ni muweza wa kila kitu."** Surat At-Tahriim: 8



63 "Ewe Mwenyezi Mungu! Niongoze mimi kwa yale ambayo watu hutofautiana kwayo katika haki kwa idhini yako. Hakika Wewe humuongoa umtakaye katika njia iliyonyooka."[2]

64 Ewe Mwenyezi Mungu! Nipe hekima ambazo mwenye kupewa hekima hizo, basi hakika atakuwa amepewa heri nyingi.[3]

65 Ewe Mwenyezi Mungu, niimarishe mimi kwa kauli iliyo thabiti katika maisha ya duniani na maisha ya Akhera.[4]

66 Ewe Mwenyezi Mungu, tupendezee imani na uipambe ndani ya nyoyo zetu, na utufanye tuuchukie ukafiri, uovu, upotovu na uasi, na utujalie kuwa miongoni mwa walioongoka.[5]

67 Ewe Mwenyezi Mungu! Nikinge na choyo ya nafsi yangu, na unijalie kuwa miongoni mwa waliofaulu.[6]

68 "Ewe Mwenyezi Mungu! Tupe hapa katika Dunia (mambo) mazuri, na Akhera utupe mazuri na utukinge kutokana na adhabu ya Moto."[7]

2- Haya yametoholewa kutoka katika Suratul-Baqarah: 213.
3- Haya yametoholewa kutoka katika Suratul-Baqarah: 269.
4- Haya yametoholewa kutoka katika Surat Ibrahim: 27.
5- Haya yametoholewa kutoka katika Suratul-Hujraat: 7.
6- Haya yametoholewa kutoka katika Surat At-Taghaabun: 16.
7- Bukhari, kwa nambari 4522, na nambari 6389, na Muslim, kwa nambari 2690.

69 Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na majaribu ya Moto na adhabu ya Moto, na kutokana na majaribu ya kaburi na adhabu ya kaburi, na kutokana na uovu wa majaribu ya utajiri, na uovu wa majaribu ya umasikini. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na uovu wa Masihi Dajali. Ewe Mwenyezi Mungu, usafishe moyo wangu kwa maji ya theluji na barafu, na utakase moyo wangu kutokana na makosa kama jinsi ulivyoitakasa nguo nyeupe kutokana na uchafu, na uweke mbali baina yangu na baina ya makosa yangu kama ulivyoweka mbali baina ya Mashariki na Magharibi. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na uvivu, madhambi na vitu vitakavyonigharimu (madeni).[8]

70 Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na kushindwa, na uvivu, na woga, na ukongwe, na ubahili, na ninajikinga kwako kutokana na adhabu ya kaburi, na kutokana na majaribu ya uhai na kifo.[9]

71 Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na balaa nzito, na kupatwa na upotofu, na hukumu mbaya, na furaha ya maadui (juu ya msiba wangu).[10]



8- Bukhari, kwa nambari 832, na Muslim, kwa nambari 589.
9- Bukhari, kwa nambari 2823, na Muslim kwa nambari 2706.
10- Bukhari kwa nambari 6347, na Muslim kwa nambari 2707, na matamshi yake ni: Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, akijikinga kutokana na kupatwa na ugumu wa balaa, na kupatwa na ususuwavu, na hukumu mbaya na furaha ya maadui (juu ya msiba wangu)."



72 Ewe Mwenyezi Mungu nitengenezee dini yangu ambayo ndiyo kinga ya jambo langu, na unitengenezee dunia yangu ambayo kunapatikana maisha yangu, na unitengenezee Akhera yangu ambako kunapatikana kuishi kwangu milele, na unijalie ziada ya uhai kwenye kila lenye heri, na ujalie kifo ni kitulizo changu kutokana na kila shari.[11]

73 Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba uongofu, ucha Mungu, kujizuia na machafu na kuwa ni mwenye kutosheka.[12]

74 Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na kushindwa, na uvivu, na uoga, na ubahili, na ukongwe, na adhabu ya kaburi. Ewe Mwenyezi Mungu, ipe nafsi yangu ucha Mungu wake na uitakase, kwani Wewe ndiye mbora wa kuitakasa. Wewe ndiye msimamizi wake na Mola wake. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na elimu isiyo na manufaa, na moyo usionyenyekea, na nafsi isiyotosheka na maombi yasiyoitikiwa.[13]

75 Ewe Mwenyezi Mungu, niongoze na unipe msimamo wa sawasawa. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba uongofu na msimamo wa sawasawa.[14]

11- Imepokelewa na Muslim, kwa nambari 2720.
12- Imepokelewa na Muslim, nambari (2721).
13- Imepokelewa na Muslim, nambari (2722).
14- Imepokelewa na Muslim, nambari (2725).

76 Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na kuondokewa neema zako, na kubadilika kwa salama yako, na kufikiwa ghafla na adhabu zako, na kila aina ya hasira zako.[15]

77 Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na uovu wa yale niliyofanya, na kutokana na uovu wa yale nisiyoyafanya.[16]

78 Ewe Mwenyezi Mungu, ziongeze mali zangu, na watoto wangu, na unibariki mimi kwa kile unachonipa. [Na refusha maisha yangu katika kukutii Wewe. Na yafanye matendo yangu kuwa mazuri], na nisamehe.[17,18]



15- Imepokelewa na Muslim, nambari (2739). , 16- Imepokelewa na Muslim, nambari (2716).

17- Ameipokea Bukhari katika kitabu chake kiitwacho "Al-Adabu Al-Mufrad" kwa nambari 653. Al-Albaaniy alisema kwamba ni hadithi sahihi katika kitabu kiitwacho "Silsilatul-Ahaadiithi As-Swahiihaa" kwa nambari 2241, na katika "Swahih Al-Adabil-Mufrad" ukurasa 244. Na yale yaliyo baina ya mabano yanaashiriwa na kauli yake Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, alipoulizwa: Ni watu gani walio bora? Akasema: "Ni yule ambaye umri wake utakuwa mrefu na matendo yake yakawa mazuri." Ameipokea hadithi hii At-Tirmidhiy kwa nambari 2329 na Ahmad kwa nambari 17716. Al-Albaaniy alisema kwamba ni hadithi sahihi katika "Swahih At-Tirmidhiy" 2/271. Nilimuuliza shekhe wetu Ibn Baaz, Mwenyezi Mungu amrehemu, juu ya kuomba kwa maombi hayo, je ni sunnah? Akasema: "Ndiyo."

18- Haya yanaashiriwa na maombi ya Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, aliyomuombea Anas: "Ewe Mwenyezi Mungu, muongezee mali zake, na watoto wake, na mbariki katika kile ulichompa." Ameipokea hadithi hii Bukhari kwa nambari 1982, na Muslim kwa nambari 660.

79 Hapana mungu apasaye kuabadiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, Mkuu, Mpole. Hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa Kiti Kikuu cha Enzi. Hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa mbingu na Mola Mlezi wa ardhi, na Mola Mlezi wa Kiti Kitukufu cha Enzi.[19]

80 Ewe Mwenyezi Mungu, rehema zako ndizo ninazozitarajia. Basi usiniache kujitegemea mwenyewe kwa kiasi cha mpepeso wa jicho, na unitengenezee mambo yangu yote. Hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe.[20]

81 Hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki ila Wewe, utakasifu ni wako. Hakika mimi nilikuwa katika madhalimu.[21]



19- Bukhari nambari 6345, na Muslim nambari 2730.
20- Ameipokea Abu Daud kwa nambari 5090, na Ahmad 5/42, na Al-Albaaniy akasema kwamba ni nzuri katika "Swahih Abi Daud" 3/250, na katika "Swahih Al-Adabil-Mufrad, kwa nambari 260, na vilevile mwanazuoni mkubwa Ibn Baaz alisema kwamba mlolongo wa wasimulizi wake ni mzuri katika kitabu kiitwacho "Tuhfatul-Akhyaar" ukurasa wa 24.
21- Tirmidhi nambari 3505, na Al-Hakim na akasema kwamba ni hadithi sahihi, na Imam Adh-Dhahaby akakubaliana naye katika hilo 1/505. Vile vile, Al-Albaaniy alisema kwamba ni hadithi sahihi katika "Swahih At-Tirmidhi 3-168, na matamshi yake ni: Maombi ya dhin nuun pindi alipomuomba Mwenyezi Mungu ilhali yuko ndani ya tumbo la chewa: An laa ilaha illa anta sub-haanaka inni kuntu minadhdhwaalimiin (Hapana mungu ila Wewe. Hakika mimi nilikuwa katika madhalimu). Kwani, hataomba mtu Muislamu kwa maombi haya katika kitu chochote kile isipokuwa Mwenyezi Mungu atamuitikia maombi yake.



82

Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ni mja wako, mtoto wa mja wako, mtoto wa kijakazi wako. Nywele zangu za utosi zipo mkononi mwako. Hukumu zako kwangu ni zenye kupita, na maamuzi yako kwangu ni ya uadilifu. Ninakuomba kupitia kila jina lako, ulilojiita kwalo mwenyewe, au uliloteremsha ndani ya Kitabu chako, au ulilomfundisha yeyote katika viumbe wako, au ulilificha ndani ya elimu ya ghaibu iliyo kwako, kwamba uifanye Qur'ani ndiyo kitulizo cha moyo wangu, na mwangaza wa kifua changu, na kiondoshaji cha huzuni yangu, na kimalizaji cha msongo wa mawazo yangu.[22]

83 Ewe Mwenyezi Mungu, Mwenye kuzigeuza nyoyo, geuza nyoyo zetu kwenye utiifu wako.[23]

84 Ewe Mwenye kuzigeuza nyoyo, uimarishe moyo wangu katika Dini yako.[24]

85 Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba unipe salama Duniani na Akhera.[25]

22- Ahmad nambari 1/391-452, Al-Haakim nambari 1/509, na Al-Haafidh Ibn Hajar akasema kwamba ni hadithi nzuri katika "Takhriij Al-Adhkaar", na vile vile Al-Albaaniy akasema kwamba ni hadithi sahihi katika "Takhriij Al-Kalim At-Twayyib" ukurasa wa 73.
23- Ameipokea Muslim kwa nambari 2654.
24- At-Tirmidhi kwa nambari 3522, na Ahmad 4/182, na Al-Haakim 1/525-528 na akasema kwamba ni Hadithi sahihi, na Adhdhahabiy akakubaliana naye, na Al-Albaaniy akasema kwamba ni hadithi sahihi "Swahiih Al-Jaamii", 6/309, na katika "Swahiih At-Tirmidhi" 3/171. Alisema Ummu Salama, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: Haya ndiyo maombi aliyokuwa Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, akiyaomba sana.5
25- Ameipokea At-Tirmidhi kwa nambari 3514, na Bukhari katika "Al-Adabul-Mufrad" kwa nambari 726, na tamshi lake kwa upokezi wa Tirmidhi ni: "Muombeni Mwenyezi Mungu salama katika dunia na akhera." Na katika tamshi lingine: "Muombeni Mwenyezi Mungu msamaha na salama, kwani mmoja wenu hakupewa baada ya yakini kilicho bora kuliko kuwa salama." Al-Albani alisema kwamba ni hadithi sahihi katika "Swahiih Ibn Majah" 3/180 na 3/185, na 3/170, na ina ushahidi mbalimbali, utazame ushahidi huo katika "Musnad Imam Ahmad" kwa upangiliaji wa Ahmad Shaakir, 1/156-157.

86 "Ewe Mwenyezi Mungu, ufanye mwisho wetu kuwa mzuri katika mambo yetu yote, na tukinge kutokana na hizaya ya dunia na adhabu za akhera." [26]

87 "Mola wangu Mlezi, nisaidie na wala usiwasaidie wengine dhidi yangu. Na ninusuru na wala usiwanusuru wengine dhidi yangu. Na wafanyie vitimbi kwa niaba yangu (maadui zangu), na wala usifanye vitimbi dhidi yangu. Na niongoze na ufanye wepesi uongofu kwangu. Na ninusuru dhidi ya kila aliyevuka mipaka dhidi yangu. Mola wangu Mlezi, nifanye niwe ni mwenye kukushukuru, mwenye kukutaja, mwenye kukuogopa, mwingi wa utiifu kwako, niwe mwenye kukunyenyekea, kurudi kwako sana. Mola wangu Mlezi, nikubalie toba yangu, na yatakase madhambi yangu, na niitikie maombi yangu, na imarisha hoja zangu, na uongoze moyo wangu, na upe ulimi wangu msimamo wa sawasawa, na niondoshee husuda ndani ya moyo wangu.".[27]

88 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika sisi tunakuomba heri alizokuomba kwazo nabii wako Muhammad - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, - na tunajikinga kwako kutokana na shari alizojikinga kwako nabii wako Muhammad - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - na Wewe ndiye mwenye kutakwa msaada, na ni juu yako kufikisha tu, na hapana uwezo wala nguvu isipokuwa ni kwa Mwenyezi Mungu."[28]



26- Ahmad 4/181, na Twabaraniy katika kitabu kiitwacho "Al-Kabiir" 2/33/1169, na katika "Dua" kwa nambari 1436, na Ibn Hibaan kwa nambari 2424, 2425 katika (Mawaarid). Alisema Al-Haafidh Al-Haithamiy katika "Majmaa Az-Zawaaid" 10/178: "Wapokezi wa Ahmad na moja ya mtiririko wa wasimulizi wa Twabaraniy ni wa kuaminika."

27- Bukhari katika "Al-Adabul-Mufrad" nambari 664-665, na Abu Daud nambari 1510-1511, Tirmidhiy nambari 3551, na Ibn Maajah nambari 3830, na Ahmad 1/127 na Al-Haakim na akasema kwamba ni sahihi, na Adh-Dhahabiy akakubaliana naye katika hilo, 1-519, naye Al-Albaniy akasema pia kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahih Abi Daud" 1/414, na katika "Sahih At-Tirmidhiy" 3/178.

28- At-Tirmidhiy nambari 3521, na Ibn Maajah nambari 3846 kwa maana yake. Alisema At-Tirmidhiy: Hadithi hii ni nzuri, na si ya kawaida (Hasanun Ghariib). Na Al-Albaani akasema kwamba ni hadithi dhaifu katika kitabu kiitwacho "Dhaif At-Tirmidhiy" ukurasa wa 387.

84 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na shari za masikio yangu, na kutokana na shari za macho yangu, na kutokana shari za ulimi wangu, na kutokana na shari za moyo wangu, na kutokana na shari za matamanio yangu."[29]

85 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na ukoma, na mbaranga, na wendawazimu, na kutokana na maradhi mabaya."[30]

86 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na tabia mbovu, na matendo mabaya, na matamanio mabaya."[31]

87 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika Wewe ni Msamehevu, Mkarimu, unapenda kusamehe, basi nisamehe."[32]



29- Abu Daud kwa nambari 1551, na Tirmidhiy kwa nambari 3492, na Nasaai kwa nambari 5470, na wengineo. Alisema Al-Albaaniy kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahih At-Tirmidhiy" 3/166, na katika "Sahih An-Nasaai" 3/1108.
30- Abu Daud kwa nambari 1554, na Nasaai kwa nambari 5493, na Ahmad 3/192, na Al-Albaaniy alisema kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahihi An-Nasaai" 3/1116, na katika "Sahih At-Tirmidhiy" 3/184.
31- At-Tirmidhiy kwa nambari 3591, na Ibn Hibaan kwa nambari 2422 (Mawaarid), na Al-Haakim 1/532, na Twabaraaniy katika kitabu kiitwacho "Al-Kabiir" 36/19/19, na Al-Albaaniy akasema kwamba ni hadithi sahihi katika kitabu kiitwacho "Sahih At-Tirmidhiy" 3/184.
32- At-Tirmidhiy kwa nambari 3513, na An-Nasaai katika kitabu cha "Al-Kubraa" kwa nambari 7712, na Al-Albaaniy alisema kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahih At-Tirmidhiy" 3/170.

88 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba kufanya matendo yenye heri, na kuacha mambo yenye kuchukiza, na kuwapenda masikini, na unifutie madhambi yangu, na unirehemu. Unapokusudia kuwajaribu watu, basi nifishe hali ya kuwa si mwenye kutiwa katika majaribu hayo. Na ninakuomba kukupenda, na kumpenda anayekupenda, na kupenda matendo yanayonisongeza kwenye mapenzi yako."[33]

89 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba (unipe) katika heri zote; zile za haraka na zinazochelewa, kwa ninayoyajua na nisiyoyajua. Na ninajikinga kwako kutokana na shari zote zinazokuja haraka na zinazochelewa, ninazozijua na nisizozijua. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba (unipe) miongoni mwa heri alizokuomba kwazo mja wako na nabii wako, na ninajikinga kwako (uniepushe) kutokana na shari alizojikinga kwako mja wako na nabii wako. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba Pepo, na yanayomtia mtu karibu yake miongoni mwa kauli au matendo, na ninajikinga kwako kutokana na Moto na yanayomtia mtu karibu yake miongoni mwa kauli au matendo, na ninakuomba ujalie kila hukumu utakayonihukumia iwe ni heri."[34]

33- Ameipokea Ahmad kwa tamko la Hadithii hii 5/243, na At-Tirmidhiy kwa nambari 3235 kwa mfano wa Hadithi hii, na akasema kwamba ni hadithi nzuri, na akasema: "Nimemuuliza Muhammad Ibn Ismail - akimkusudia Bukhari - akasema: 'Hadithi hii ni nzuri tena sahihi (Hasanun Sahih)." Na mwisho wa Hadithi akasema Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: "Hayo ni haki, basi yasomeni na mjifunze." Na Al-Haakim 1/521, naye Al-Albaaniy akasema kwamba ni Hadithi sahihi katika "Sahih At-Tirmidhiy" 3/318.

34- Ameipokea Abu Daud kwa nambari 3846 kwa matamshi ya Hadithi hii hii, na Ahmad 6/134 na matamshi ya ziada ya pili, imepokelewa na Al-Haakim na akasema kwamba ni sahihi, na Adh-Dhahaby akakubaliana naye 1/521, na matamshi ya ziada ya kwanza ni mapokezi yake. Vile vile Al-Albaaniy alisema kwamba ni Hadithi sahihi katika "Sahih Ibn Maajah" 2/327.

90

"Ewe Mwenyezi Mungu, nihifadhi kwa Uislamu nikiwa nimesimama. Na nihifadhi kwa Uislamu nikiwa nimekaa. Na nihifadhi kwa Uislamu nikiwa nimelala. Na usinijalie kuwa ni mwenye kufurahikiwa na adui zangu au hasidi wangu kwa sababu ya misiba yangu. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba (unipe) kutoka katika kila heri ambayo hazina zake ziko mkononi mwako. Na ninajikinga kwako kutokana na kila shari ambayo hazina zake ziko mkononi mwako."[35]

91 "Ewe Mwenyezi Mungu, tugawie sehemu katika kukuogopa ambayo kwayo utazuia baina yetu na kukuasi. Na katika kukutii ambako kwa hilo utatufikisha katika Pepo yako. Na yakini ambayo kwayo utatupunguzia matatizo ya dunia. Ewe Mwenyezi Mungu, tustareheshe kupitia masikio yetu na macho yetu na nguvu zetu kwa muda ambao utatupa uhai. Na uvijalie viwe ni vyenye kubakia. Na ujalie kisasi chetu juu ya wenye kutudhulumu. Na utunusuru dhidi ya aliyetufanyia uadui. Na usijalie matatizo yetu kuwa katika dini yetu. Na usiifanye dunia kuwa ndiyo jambo muhimu zaidi kwetu, wala kuwa ndiyo kiwango cha juu zaidi cha elimu yetu, wala usimpe mamlaka juu yetu mtu asiyetuhurumia."[36]



35- Al-Haakim 1/525 na akasema ni hadithi sahihi, na Adh-Dhahabiy akakubaliana naye. Vile vile, Al-Albaaniy alisema ni hadithi nzuri (Hasan) katika "Sahihi Al-Jaamii" 2/398, na katika "Silsilat Al-Ahaadiith Asswahiiha" 4/54 kwa nambari 1540.

36- At-Tirmidhiy kwa nambari 3502, na Al-Haakim 1/528 na akasema kwamba ni sahihi, na Adh-dhahabiy akakubaliana naye, vile vile Ibn Sunniy kwa nambari 446. Na Al-Albaaniy akasema kwamba ni Hadithi nzuri (Hasan) katika "Sahih At-Tirmidhiy" 3/168 na katika kitabu kiitwacho "Sahih Al-Jaamii" 1/400.

92 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na uoga, na ninajikinga kwako kutokana na ubahili, na ninajikinga kwako kutorudi kwenye umri wenye udhalili, na ninajikinga kwako kutokana na majaribu ya dunia na adhabu za kaburi."[37]

93 "Ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe makosa yangu, na ujinga wangu, na kupindukia kwangu mipaka katika mambo yangu, na kwa yale ambayo Wewe unayafahamu zaidi kuliko mimi. Ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe mambo ninayoyafanya kwa mzaha, na kwa kuyapa uzito, na kwa kukosea, na kwa kukusudia, na yote hayo ni juu yangu."[38]

94 **"Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi nimeidhulumu nafsi yangu dhuluma nyingi, na hakuna wa kufuta madhambi isipokuwa Wewe. Basi nisamehe msamaha utokao kwako, na unihurumie. Hakika Wewe ni Msamehevu, Mwingi wa kurehemu."[39]**

95 "Ewe Mwenyezi Mungu, nimejisalimisha kwako, na kwako nimeamini, na juu yako nimetegemea, na kwako nimejisogeza, na kwa ajili yako ninapambana. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwa utukufu wako, hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe, kwamba usije nipoteza. Wewe ndiye uliye hai ambaye hafi, na majini na watu wanakufa."[40]



96 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika sisi tunakuomba sababu za kupata rehema zako, na sababu zitakazotia nguvu kupata msamaha wako, na kupata salama kutokana na kila dhambi, na kupata faida katika kila wema, na kufaulu kuipata Pepo na kuokoka kutokana na Moto."[41]

37- Bukhari kwa nambari 2822.
38- Wamekubaliana juu ya usahihi wa Hadithi hii, Bukhari kwa nambari 6398 na Muslim kwa nambari 2719.
39- Wamekubaliana juu ya usahihi wa Hadithi hii, Bukhari kwa nambari 834, na Muslim nambari 2705.
40- Wamekubaliana juu ya usahihi wa Hadithi hii, Bukhari kwa nambari 6398 na Muslim kwa nambari 2719.
41- Ameipokea Al-Haakim 1/525 na akasema kwamba ni sahihi, na Adh-Dhahabiy akakubaliana naye, na Al-Baihaqi katika "Ad-Da'awaat" kwa nambari 206. Pia angalia kitabu "Al-Adhkaar" cha imamu Annawawiy ukurasa wa 340. Mhakiki Abdul-Qaadir Al-Arnaautu alisema kwamba ni hadithi nzuri (Hasan).



97 "Ewe Mwenyezi Mungu, wasamehe Waumini wa kiume na wa kike."[42]

98 "Ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe madhambi yangu, na unipanulie katika nyumba yangu, na unibariki kwa kile unachoniruzuku."[43]

99 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba katika fadhila zako na rehema zako. Hakika hakuna anayemiliki hayo isipokuwa Wewe."[44]

100 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na ukongwe (uzee uliopindukia), na kuporomoka kutoka sehemu za juu, na kudondokewa na jengo, na huzuni, na kuzama majini, na kuungua kwa moto. Na ninajikinga kwako kutochezewa na shetani wakati wa kifo. Na ninajikinga kwako nisife kwenye njia yako hali ya kuwa ni mwenye kurudi nyuma. Na ninajikinga kwako nisife kwa kuumwa na nyoka au mfano wake."[45]

101 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na njaa. Kwani njaa ndiyo mwenza mbaya wa kulala naye. Na ninajikinga kwako kutokana na hiyana. Kwani hiyana ndiyo rafiki mbaya zaidi."[46]

42- Haya yatokana na Hadithi ya Ubadah - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - kwamba alisema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu - rehema na amani ziwe juu yake - akisema: "Atakayewatakia msamaha Waumini wanamume na wanawake, Mwenyezi Mungu atamuandikia jema kwa kila Muumini wa kiume na wa kike." Ameipokea At-Twabaraany katika kitabu "Al-Kabiir" 5/202 kwa nambari 5092, na 3/334 na kwa nambari 2155. Al-Haithamy alisema kwamba mtiririko wa mapokezi yake ni mzuri katika kitabu "Majmaa' Az-zawaaid", 10/210. Na Al-Albaaniy akasema kwamba ni hadithi nzuri (Hasan) katika "Sahihi Al-Jaamii" kwa nambari 5902, 5/242.

43- Ameipokea Ahmad, kwa nambari 16599, na kwa nambari 23114, na kwa nambari 23188, naye At-Tirmidhiy kwa nambari 3500, na wamesema waliokihakiki kitabu kiitwacho "Al-musnad" kwamba ni Hadithi nzuri (hasan) kwa sababu ya hadithi nyinginezo na mfano wake, 27/144, na katika 38/197, na katika 38/145.

44- Ameipokea Hadithi hii At-Twabaraniy. Na amesema Al-Haithamiy katika kitabu "Majmau Az-zawaaid", 159/10: "Wapokezi wake ni wapokezi wa vitabu vya hadithi sahihi isipokuwa Muhammad Ibn Ziad, naye anaaminika". Vile vile, Al-Albaaniy amesema kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahih Al-Jaamii", 404/1, kwa nambari 1278.

45- Ameipokea Hadithi hii Abuu Daud kwa nambari 1552, na An-Nasaai kwa nambari 5531, na kwa nambari 5532, na Al-Albaani alisema kwamba ni sahihi katika "Sahihi An-Nasaai", 3/1123, na katika "Sahihi sunan Abi Daud" 1/425.

46- Ameipokea Hadithi hii Abuu Daud kwa nambari 1547, na An-Nasaai kwa nambari 5483. Albaani alisema kwamba ni hadithi nzuri (Hasan) katika "Sahih An-Nasaai" 1112/3.



102 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na kushindwa, na uvivu, na uoga, na ubahili, na ukongwe, na ugumu wa moyo, na kughafilika, na umasikini, na udhalili, na ufukara uliopindukia, na ukafiri, na kuvuka mipaka, na kutotii, na unafiki, na kutaka kusikika, na kujionyesha, na ninajikinga kwako kutokana na uziwi, na ububu, na wendawazimu, na ukoma, na mbaranga, na maradhi mabaya."[47]

103 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na ufakiri (umasikini uliopindukia), na uchache, na udhalili, na ninajikinga kwako kutodhulumu au kudhulumiwa."[48]

104 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na jirani muovu katika makazi yangu ya kudumu, kwani jirani wa kijijini (safarini) huhama (humalizika ujirani wake)."[49]

47- Ameipokea Hadithi hii An-Nasaai kwa nambari 5493, na Al-Haakim 1/530. Albaani alisema kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahih Al-Jaami'i" 406/1, na katika kitabu "Irwaaul-Ghaliil" kwa nambari 852.

48- Ameipokea Hadithi hii Abu Daud kwa nambari 1544, na An-Nasaai kwa nambari 5475, na amesema Albani kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahihi An-Nasaai" 3/1111, na katika "Sahihi Al-Jaami'i" 1/407, na yaliyo kwenye mabano yamepokelewa kwa Ibn Hibaan (Mawaarid), vile vile Albaaniy amesema ni Hadithi sahihi katika "Sahih Mawaarid Adh-Dhamaan 2/455.

49- Bukhari katika "Al-Adab Al-Mufrad" kwa nambari 117, na Al-Haakim 1/532 na akasema kwamba ni Hadithi sahihi, na Adh-Dhahabi akakubaliana naye. Vile vile ameipokea Hadithi hii An-Nasaai kwa nambari 5517, na Albaaniy akasema kwamba ni Hadithi sahihi katika "Sahih Al-Jaami" 1/408 na vile vile katika "Sahih An-Nasaai" 3/1118.



105 **"Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na moyo usiokuwa na hofu, na kutokana na maombi yasiyojibiwa, na kutokana na nafsi isiyotosheka, na kutokana na elimu isiyo na manufaa, na ninajikinga kwako na mambo haya manne."[50]**

106 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na siku mbaya, na usiku mbaya, na wakati mbaya, na mwenza mbaya, na kutokana na jirani muovu katika makazi yangu ya kudumu."[51]

107 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba Pepo, na ninajikinga kwako kutokana na Moto" (utayasema mara tatu).[52]

108 "Ewe Mwenyezi Mungu, nipe ufahamu wa dini."[53]

109 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako nisije kukushirikisha kwa jambo ninalolijua, na ninakutaka msamaha kwa nisilolijua."[54]

50- Ameipokea Hadithi hii At-Tirmidhi kwa nambari 3482, na Abu Daud kwa nambari 1549, na Albaani akasema kwamba ni Hadithi sahihi katika kitabu "Sahih Al-Jaami'i" kwa nambari 1295, na vile vile katika "Sahih An-Nasaai" 3/1113.

51- Ameipokea hadithi hii At-Twabarani na akasema Al-Haithami katika kitabu "Az-Zawaaid" 144/10 kwamba: "Wapokezi wake ni wapokezi wa vitabu vya hadithi sahihi", na Albaaniy akasema kwamba ni hadithi nzuri (Hasan) katika kitabu "Sahih Al-Jaami" 1/411, kwa nambari 1290.

52- Ameipokea Hadithi hii At-Tirmidhi kwa nambari 2572, na Ibn Majah kwa nambari 3340, na An-Nasaai kwa nambari 5536, na Albaani akasema kwamba ni hadithi sahihi katika kitabu "Sahih At-Tirmidhiy" 2/319, na katika kitabu "Sahih An-Nasaai" 3/1121, na matamshi ya Hadithi yake ni: "Atakayemuomba Mwenyezi Mungu Pepo mara tatu, Pepo itasema: 'Ewe Mwenyezi Mungu, muingize Peponi.' Na atakayejikinga kwa Mwenyezi Mungu kutokana na Moto mara tatu, Moto utasema: 'Ewe Mwenyezi Mungu, mkinge kutokana na Moto.'"

53- Hili linaashiriwa na Hadithi ya upokezi wa Bukhari na Muslim katika maombi ya Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - aliyomuombea bin Abbas, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na juu ya baba yake. Ameipokea Bukhari kwa nambari 143, na Muslim kwa nambari 2477.

54-Ameipokea Hadithi hii Ahmad 4/403, na Ibn Abi Shaibah 10/337, na At-Twabaraniy katika "Al-Muujamul-Ausatwi" 4/284, na Albaani akasema kwamba ni Hadith nzuri (Hasan) katika "Sahih At-Targhiib wat-Tarhiib" 1/19.

110 **"Ewe Mwenyezi Mungu, ninufaishe kwa uliyonifundisha, na unifundishe yenye manufaa kwangu, na unizidishie elimu."**[55]

111 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba elimu yenye manufaa, na riziki nzuri, na matendo yenye kukubalika."[56]

112 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba Ewe Mwenyezi Mungu kwa kuwa Wewe ni Mmoja, wa Pekee, Mkusudiwa, ambaye hakuzaa wala hakuzaliwa na wala hana yeyote wa kufananishwa naye, kwamba unisamehe madhambi yangu. Hakika Wewe ni Msamehevu, Mrehemevu."[75]

113 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba kwa kuwa sifa njema zote ni zako, hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe [uliye mpweke usiye na mshirika], Mwenye kuneemesha mno. [Ewe] Muumbaji mwanzilishi wa mbingu na ardhi. Ewe mwenye utukufu na ukarimu. Ewe uliye Hai, ewe Msimamia yote milele. Hakika mimi ninakuomba Pepo na ninajikinga kwako kutokana na Moto."[58]



55- Ameipokea Hadithi hii At-Tirmidhi kwa nambari 3599, na Ibn Maajah kwa nambari 259, na Albaani amesema kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahih Ibn Maajah" 1/47.
56- Ameipokea Hadithi hii Ibn Maajah kwa nambari 925, na An-Nasaai katika "Amali al-yaumi wal-lailah" kwa nambari 102, na Ahmad 6/294, na 305, na Albaani alisema kwamba ni hadithi sahihi katika kitabu "Sahih Ibn Maajah" 1/152.
57- Ameipokea Hadithi hii An-Nasaai kwa nambari 1300, na matamshi ya Hadithi hii ni yake, na vile vile An-Nasaai katika "Al-Kubraa" kwa nambari 7665, na Abu Daud kwa nambari 985, na Albaani akasema kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahih Sunan An-Nasaai", 1/147.
58- Ameipokea Abu Daud kwa nambari 1495, na Ibn Majah kwa nambari 3858, na An-Nasaai kwa nambari 1299, na At-Tirmidhiy kwa nambari 3544, na Albaani alisema kwamba ni Hadithi sahihi katika "Sahih An-Nasai" 1/279, na katika "Sahih Ibn Majah" 2/329.

114 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba kwa kuwa ninashuhudia kuwa Wewe ni Mwenyezi Mungu, hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe, uliye wa Pekee, Mkusudiwa, ambaye hakuzaa wala hakuzaliwa na wala hakuna yeyote wa kufananishwa naye."[59]

115 "Ewe Mola wangu Mlezi, nisamehe, na nikubalie toba yangu. Hakika Wewe ni Msamehevu, Mfuta madhambi."[60]

116 "Ewe Mwenyezi Mungu, kwa elimu yako ya mambo yaliyojificha, na kwa uwezo wako juu ya viumbe, nipe uhai maadamu unajua kuwa uhai ni heri kwangu, na unifishe maadamu unajua kuwa kifo ni heri kwangu. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba unifanye kukuhofu kwa wazi na kwa siri, na ninakuomba neno la haki katika hali ya kuridhia na hasira, na ninakuomba kuwa na msimamo sahihi kwenye hali ya utajiri na umasikini, na ninakuomba neema zisizomalizika, na ninakuomba kitulizo cha jicho kisichokatika, na ninakuomba kuridhia baada ya kupita hukumu, na ninakuomba maisha ya utulivu baada ya kifo, na ninakuomba ladha ya kutazama uso wako, na shauku ya kukutana na Wewe, bila ya madhara yenye kudhuru, wala majaribu yenye kupoteza. Ewe Mwenyezi Mungu, tupambe kwa pambo la imani, na utufanye kuwa viongozi wa walioongolewa."[61]



59- Abuu Daud kwa nambari 985, na At-Tirmidhy kwa nambari 3475, na Ibn Majah kwa nambari 3857, na Ahmad 5/360, na Albaani alisema kwamba ni Hadithi sahihi katika "Sahih Sunan At-Tirmidhiy" 3/163.
60- Abu Daud kwa nambari 1518, na At-Tirmidhi kwa nambari 3434, na matamshi haya ni ya hadithi yake, na ameipokea An-Nasai katika "Al-Kubraa" kwa nambari 10292, na Ibn Majah kwa nambari 3814, na Albaani alisema kwamba ni Hadithi sahihi katika "Sahih Ibn Majah" 2/321, na "Sahih At-Tirmidhiy" 3/153.
61- Ameipokea An-Nasai kwa nambari 1305, na Ahmad 4/264, na Albaani alisema kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahih An-Nasai" 1/280 na 1/281.

106 "Ewe Mwenyezi Mungu, niruzuku kukupenda, na kupenda yule ambaye kumpenda kutaninufaisha kwako. Ewe Mwenyezi Mungu, fanya katika kile ulichoniruzuku miongoni mwa ninachopenda kuwa ni nguvu kwangu kwa kile unachokipenda. Ewe Mwenyezi Mungu, fanya katika kile ulichonikunjia miongoni mwa vile ninavyovipenda kuwa chenye kunipa muda wa kufanya kile unachokipenda."[62]

107 "Ewe Mwenyezi Mungu, nitakase kutokana na madhambi na makosa. Ewe Mwenyezi Mungu, nitakase kutokana na madhambi kama jinsi inavyotakaswa nguo nyeupe kutokana na uchafu. Ewe Mwenyezi Mungu, nisafishe kwa theluji na kwa maji, na kwa barafu."[63]

108 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na ubahili, na uoga, na umri mbaya, na majaribu ya kifua, na adhabu za kaburi."[64]

109 "Ewe Mwenye Mungu, Mola Mlezi wa Jibril, na Mikail, na Israfiil, ninajikinga kwako kutokana na joto la Moto, na kutokana na adhabu ya kaburi."[65]

108 "Ewe Mwenyezi Mungu, nijaze uongofu wangu, na unikinge kutokana na shari ya nafsi yangu."[66]

109 "Ewe Mwenye Mungu, hakika mimi ninakuomba elimu yenye manufaa, na ninajikinga kwako kutokana na elimu isiyo na manufaa." [67]

62- Ameipokea At-Tirmidhi kwa nambari 3491 na akasema kwamba ni Hadithi nzuri (Hasan), na Sheikh Abdul-Qaadir Al-Arnaut alisema: "Nayo ni kama alivyosema." Angalia uhakiki wake kwenye "Jaamii Al-Usuul", 4/341.

63- Ameipokea Hadithi hii Muslim kwa nambari 476, na An-Nasai kwa nambari 400.

64- Ameipokea An-Nasai kwa nambari 5469 na matamshi ya hadithi yake ni: "Alikuwa Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - akijikinga kutokana na mambo matano: Kutokana na ubahili, na uoga, na umri mbaya, na majaribu ya kifua, na adhabu za kaburi." Vile vile, ameipokea Abu Daud kwa nambari 1539, na Al-Arnaut akasema kuwa ni hadithi nzuri katika kubainisha kwake upokezi wa Hadithi za kitabu "Jaami'ul-Usuul" 4/363.

65- Ameipokea An-Nasai kwa nambari 1344, na Ahmad 6/61, na Al-Baihaqi katika "Ad-Daawaat" kwa nambari 109, na Albaani akasema kwamba ni Hadithi sahihi katika "Sahih An-Nasai" 3/1121, na katika "Silsilatul-Ahadithi As-Swahiihah" kwa nambari 1544.

66- Ameipokea At-Tirmidhiy na matamshi ya hadithi hii ni yake 5/519 kwa nambari 3483, na ameipokea Ahmad 33/197 kwa nambari 19992, na Al-Haakim 1/510 kwa mfano wake vile vile, na akasema kwamba ni hadithi sahihi, na Adh-Dhahabii akakubaliana naye. Walisema wahakiki wa mtiririko wa mapokezi ya "Al-Musnad" kuhusu hadithi ya Ahmad 33/197: "Mtiririko wa wapokezi wake ni sahihi kwa masharti ya Bukhari na Muslim". Na ama matamshi ya hadithi ya At-Tirmidhiy, hayo ameyadhoofisha Albaaniy katika "Dhaif At-Tirmidhiy" ukurasa wa 379.

67- Ameipokea An-Nasai katika kitabu cha "Al-Kubraa" kwa nambari 7867, na Ibn Majah kwa nambari 3843, Albani alisema kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahihi Sunan Ibn Majah" 2/327, na matamshi ya Hadithi yake ni: "Muombeni Mwenyezi Mungu elimu yenye manufaa na mjikinge kwa Mwenyezi Mungu kutokana na elimu isiyokuwa na manufaa."

110 "Ewe Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa mbingu (saba) na Mola Mlezi wa ardhi, na Mola Mlezi wa Kiti cha Enzi kitukufu, Mola wetu Mlezi na Mola Mlezi wa kila kitu, Mwenye kupasua mbegu na kokwa, na Mwenye kuteremsha Taurati na Injili na Qur'ani, ninajikinga kwako kutokana na shari ya kila kitu ulichokishika kwa nywele za utosi. Ewe Mwenyezi Mungu, Wewe ndiye wa Mwanzo hakuna kitu kabla yako, na Wewe ndiye wa Mwisho hakuna kitu baada yako, na Wewe ni wa Wazi hakuna kitu juu yako, na Wewe ni wa Ndani hakuna kitu chini yako, tulipie madeni na ututosheleze kutokana na ufakiri."[68]

108 "Ewe Mwenyezi Mungu, unganisha baina ya nyoyo zetu, na tengeneza mambo ya baina yetu, na tuongoze njia ya amani, na tuokoe kutoka kwenye giza kwenda kwenye mwangaza, na tukinge kutokana na uchafu unaoonekana na usioonekana, na utubariki katika usikivu wetu, na




kuona kwetu, na mioyo yetu, na wake zetu, na vizazi vyetu, na tusamehe, hakika wewe ni Msamehevu, Mrehemevu, na tufanye tuwe ni wenye kushukuru neema zako, wenye kukusifu kwa neema hizo, wenye kuzipokea, na tutimizie neema hizo."[69]

68- Ameipokea Muslim kwa nambari 2713, kutoka kwa Abu Huraira - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.

69- Ameipokea Hadithi hii Abu Daud kwa nambari 969, na Al-Haakim, na matamshi ya hadithi hii ni yake 1/265, na amesema: "Ni hadithi sahihi kwa masharti ya Muslim." Na Adh-Dhahabi alikubaliana naye katika hilo 26/1, na Albaani akasema kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahih Al-Adab Almufrad" kwa nambari 630.

109

"Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba kukuomba kwa heri, na dua ya heri, na kufaulu kwa heri, na matendo ya heri, na malipo ya heri, na maisha ya heri, na kifo cha heri, na niimarishe, na ifanye mizani yangu kuwa nzito, na nihakikishie imani yangu, na unyanyue daraja zangu, na unikubalie swala zangu, na unisamehe makosa yangu, na ninakuomba daraja za juu Peponi. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba ufunguzi wa heri, na mwisho wake, na mkusanyiko wake, na mwanzo wake, na uwazi wake, na undani wake, na daraja za juu Peponi amiin. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba heri zenye kuja, na heri za ninayofanya, na heri ninazotenda, na heri za ndani, na heri za nje, na daraja za juu Peponi, amiin. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba unyanyue utajo wangu, na uniondolee makosa yangu, na ulifanye vizuri jambo langu, na uusafishe moyo wangu, na uihifadhi tupu yangu, na utie mwangaza moyoni mwangu, na unisamehe dhambi zangu, na ninakuomba daraja za juu Peponi, amiin. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba utie baraka ndani ya nafsi yangu, na ndani ya masikio yangu, na ndani ya macho yangu, na ndani ya roho yangu, na ndani ya maumbile yangu, na ndani ya tabia yangu, na kwa watu wangu, na ndani ya uhai wangu, na ndani ya kifo changu, na ndani ya matendo yangu, nikubalie mema yangu, na ninakuomba daraja za juu Peponi, amiin"[70].




70- Ameipokea Hadithi hii Al-Haakim kutoka kwa Ummu Salama hali ya kuwa imenyanyuliwa mpaka kwa Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, 1/520, na akasema kwamba ni hadithi sahihi, na Adh-Dhahabi akakubaliana naye 1/520, na vile vile Al-Baihaqi katika kitabu "Ad-Dawaat" kwa nambari 225, na At-Twabarani katika kitabu "Al-Kabiir" 23/326, kwa nambari 717.

110 "Ewe Mwenyezi Mungu, niepushe na tabia mbovu, na matamanio mabaya, na matendo machafu, na maradhi yenye kuambukiza."[71]

111 "Ewe Mwenyezi Mungu, nifanye niridhike kwa kile unachoniruzuku, na unibariki ndani yake, na unipe kilicho heri badala ya kila kilichopotea."[72]

112 "Ewe Mwenyezi Mungu, nifanyie hesabu nyepesi (juu ya matendo)."[73]



113 "Ewe Mwenyezi Mungu, nisaidie katika kukutaja, na kukushukuru, na kukufanyia ibada kwa uzuri."[74]

114 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba imani isiyorudi nyuma, na kuwa karibu na Mtume Muhammad -rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - ndani ya Pepo za juu zenye kubakia milele."[75]

71- Ameipokea Al-Haakim 1/523 na amesema: "Ni sahihi kwa sharti la Muslim." Na Adh-Dhahabi akakubaliana naye 1/532. Na vile vile ameipokea At-Twabarani katika "Al-Mu'ujam Al-Kabiir" 19/19 kwa nambari 36, na Albaani akasema kwamba ni hadithi sahihi katika "Dhwilaal Al-Jannah" kwa nambari 13.

72- Ameipokea Al-Haakim 1/532 na akasema ni hadithi sahihi, na Adh-dhahabi akakubaliana naye 1/510, kutoka kwa Ibn Abas - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao, na vile vile ameipokea Al-Baihaqi katika kitabu "Al-Aadaab" kwa nambari 1084, na katika "Ad-Daawaat Al-Kabiir" 211, Al-Haafidh Ibn Hajar akasema kwamba ni hadithi nzuri (Hasan) katika "Al-Futuuhaat Ar-Rabaaniyya" 4/383.

73- Ameipokea Ahmad 6/48, na Al-Haakim 1/255, na akasema: "Ni sahihi kwa sharti la Muslim", na Adh-dhahabi akakubaliana naye 1/255. Amesema Aisha - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, "Pindi alipoondoka, nikasema: 'Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu, ni ipi hesabu iliyo nyepesi?' Akasema: "Ni Mwenyezi Mungu atazame ndani ya kitabu cha mja kisha amsamehe. Na hakika atakayehojiwa hesabu (ya matendo) siku hiyo ewe Aisha, basi ataangamia. Na kila kinachomsibu Muumini, Mwenyezi Mungu aliyetakasika na kutukuka humfutia makosa kwa hilo hata mwiba unaomdunga." Mwanachuoni Albaani alisema kuhusu hadithi hii katika "Mishkaat Al-Maswaabiih": Mtiririko wa mapokezi yake ni mzuri."

74- Ameipokea Ahmad 2/299, na Al-Haakim 1/499, na akasema kwamba ni hadithi sahihi, na Adh-dhahabi akakubaliana naye. Na hadithi hii ni kama walivyosema, na vile vile ipo kwa Abuu Daud kwa nambari 1524, na An-Nasaai katika kitabu "Al-Kubraa" kwa nambari 9973, na Albaani alisema kwamba ni hadithi sahihi katika "Sahih Al-Adab Al-Mufrad" kwa nambari 534.

75- Ameipokea Ibn Hibaan "Mawaarid" ukurasa wa 604, kwa nambari 2436 kutoka kwa Ibn Masud - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - mapokezi yake yakiishia kwake. Na ameipokea Ahmad katika mapokezi mengine 1/386, 400, na Nasaai katika kitabu "A'amalul-yaumi wallailah" kwa nambari 869 na Albaani akasema kwamba ni Hadithi sahihi katika "Asilsilati Al-Sahiihah" kwa nambari 2301.

115

"Ewe Mwenyezi Mungu, nikinge kutokana na shari za nafsi yangu, na nipe maazimio juu ya uongofu wa jambo langu. Ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe makosa niliyoyafanya kwa siri, na niliyoyafanya kwa wazi, na niliyoyakosea, na niliyoyakusudia, na niliyoyatambua, na nisiyoyatambua."[76]

116

"Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na kushindwa kulipa deni, na kushindwa na maadui, na kutokana na maadui zangu kufurahia misiba yangu."[77]

117

"Ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe, na uniongoze, na uniruzuku, na unipe salama. Ninajikinga kwako kutokana na ufinyu wa kisimamo siku ya Kiyama."[78]

118

"Ewe Mwenyezi Mungu, nistareheshe kwa usikivu wangu, na kuona kwangu, na yafanye macho yangu na masikio yangu ni vyenye kubakia pamoja nami, na ninusuru dhidi ya atakayenidhulumu, na nifanyie kisasi dhidi yake."[79]

119

"Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba maisha yaliyo bora, na kifo kizuri, na marejeo ya Akhera yasiyo na hizaya wala kufedhehesha."[80]

76- Ameipokea An-Nasai katika kitabu "Al-Kubraa" 6/246 kwa nambari 10830, na Al-Haakim 1/510 na akasema ni hadithi sahihi, na Adh-dhahabi akakubaliana naye. Vile vile ameipokea Ahmad 4/444, na pia iko katika "Al-Musnad Al-Muhaqqaq", 33/197, kwa nambari 19992. Alisema Al-Hafidh katika kitabu "Al-Iswaabah": Mtiririko wa mapokezi yake ni sahihi." Na Albaani alisema kwamba ni hadithi sahihi katika kitabu "Takhriij riyadhi As-Swaalihiin" alipokuwa anaielezea Hadithi nambari 1495.

77- Ameipokea An-Nasai kwa nambari 5475, na Ahmad 2/173, na Albaani akasema kwamba ni Hadithi sahihi katika "Sahih An-Nasai" 3/1113.

78- Ameipokea An-Nasai kwa nambari 1617, na Ibn Majah kwa nambari 1356, na Albani alisema kwamba ni Hadithi sahihi katika "Sahih Sunan An-Nasai" 1/356, na katika "Sahihi Ibn Majah", 1/226.

79- Ameipokea At-Tirmidhiy kwa nambari 3681, na Bukhari katika "Al-Adab Al-Mufrad" kwa nambari 650 na Al-Hakim 1/523, na akasema kwamba ni hadithi sahihi na Adh-dhahabi akakubaliana naye. Na Albaani alisema kwamba ni Hadithi sahihi katika "Sahih At-Tirmidhiy" 3/188.

80- Ameipokea hadithi hii Al-Haakimu, 1/154, na kwenye kitabu cha "Zawaaidu Musnadi Al-Bazzaar" 2/442, kwa nambari 2177, na vile vile ameipokea At-Tabaraani katika "Ad-dua'a", kwa nambari 1435, na akasema Al-Haithami katika kitabu "Majmau' Azzawaaidi", 10/179: "Mtiririko wa mapokezi ya At-Twabaraani ni mzuri."

120

"Ewe Mwenyezi Mungu, sifa njema zote ni zako. Ewe Mwenyezi Mungu, hakuna wa kukunja ulichokikunjua, wala hakuna wa kukunjua ulichokikunja, wala hakuna wa kumuongoa uliyempoteza, wala hakuna wa kumpoteza uliyemuongoa, wala hakuna wa kutoa ulichokizuia, wala hakuna wa kuzuia ulichokitoa, na wala hakuna wa kumuweka karibu uliyemuweka mbali, na wala hakuna wa kumuweka mbali uliyemuweka karibu. Ewe Mwenyezi Mungu, tukunjulie baraka zako, na rehema zako, na fadhila zako, na riziki zako. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba neema zenye kubakia ambazo hazibadiliki wala haziondoki. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba neema siku za umasikini, na amani siku za hofu. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na shari ya ulichotupa na shari ya ulichotuzuia. Ewe Mwenyezi Mungu, tufanye kuipenda imani na uipambe kwenye mioyo yetu, na utufanye kuchukia ukafiri, kuvuka mipaka na uasi, na utufanye miongoni mwa walioongoka. Ewe Mwenyezi Mungu, tufishe tukiwa ni Waislamu, na tupe uhai tukiwa ni Waislamu, na tukutanishe na waja wema bila ya kupata hizaya wala kujaribiwa. Ewe Mwenyezi Mungu, wapige vita makafiri wanaowapinga Mitume wako, na wanaozuia njia yako, na weka juu yao maangamivu yako ya adhabu zako. Ewe Mwenyezi Mungu, wapige vita makafiri waliopewa Kitabu, Wewe ndiye Mungu wa kweli, [amiin]."[81]

121

"Ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe, na unirehemu, na uniongoe, na unipe salama, na uniruzuku."[82]
"....na niunge na uninyanyue."[83]

81- Ameipokea Ahmad kwa matamshi ya hadithi hii, 3/424 na 24/246, kwa nambari 15492, na yaliyo kwenye mabano ni upokezi wa Al-Haakim 1/507, 3/23-24. Na ameipokea Bukhari katika kitabu "Al-Adab Al-Mufrad" kwa nambari 699, na Albaani akasema kwamba ni Hadithi sahihi katika "Takhriji fiqh As-Siirah" ukurasa 284, na katika "Sahih Al-Adab Al-Mufrad" cha Bukhari, kwa nambari 538, ukurasa 259.
82- Ameipokea Muslim kwa nambari 2696, na kwa nambari 2697, na katika upokezi wa Muslim: "Hakika maneno hayo yanakukusanyia dunia yako na Akhera yako" na katika Sunan Abi Daud kwa nambari 850: Alisema: "Pindi alipoondoka bedui huyo, akasema Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, "Hakika ameijaza heri mikono yake."
83- Tazama: Sunan Ibn Majah, kwa nambari 898, na Sunan At-Tirmidhi, kwa nambari 284, na Sahih Ibn Majah 1/148, na Sahih At-Tirmidhi 1/90.



122 "Ewe Mwenyezi Mungu, tuzidishie wala usitupunguzie, na ututukuze na wala usitudhalilishe, na utupe na wala usitunyime, na utupendelee na wala usipendelee wengine kuliko sisi, na uturidhishe na uturidhie."[84]

123 "Ewe Mwenyezi Mungu, ulifanya vizuri maumbile yangu, basi ifanye tabia yangu kuwa nzuri."[85]

124 "Ewe Mwenyezi Mungu, niimarishe na unifanye kuwa muongofu aliyeongolewa."[86]

125 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba kuwa imara katika mambo, na kuwa na azimio juu ya uongofu, na ninakuomba mambo yenye kuleta rehema zako, na matendo yatakayotilia nguvu kupata msamaha wako, na ninakuomba kushukuru neema zako, na kukuabudu kwa uzuri, na ninakuomba moyo uliosalimika, na ulimi unaosema kweli, na ninakuomba heri unazozijua, na ninajikinga kwako kutokana na shari unazozijua, na ninakutaka msamaha kwa unayoyajua. Hakika Wewe ndiye Mjuzi zaidi wa mambo yaliyofichikana."[87]

84- Ameipokea At-Tirmidhi 5/326 kwa nambari 3173, na Al-Haakim 2/98, na amesema Abdul Qaadir Al-Arnautu kwamba ni Hadithi sahihi na nzuri (Hassan) katika uhakiki wake kwenye kitabu "Jaamii Al-Usuul" 11/282 kwa nambari 8847.

85- Ameipokea Ahmad 6/68/6 na 155, na 1/403 na Ibn Hibaan (2423-Mawaarid) na At-Twayaalisi 374, na Musnad Abi Ya'alaa kwa nambari 5075, na amesema Albani kwamba ni Hadithi sahihi katika "Irwaai Al-Ghaliil" 1/115, kwa nambari 74.

86- Hii imeashiriwa na maombi ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, akimuombea Jariri - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Angalia: Bukhari kwa nambari 6333, na vile vile kwa nambari 3020, 3036, na nyinginezo.

87- Ameipokea Ahmad 28/338, kwa nambari 17114, na 28/356, kwa nambari 17133, na Tirmidhi kwa nambari 3407, na At-Tabarani katika kitabu "Al-Muujamu Al-Kabiir" kwa matamshi ya Hadithi hii kwa nambari 7135, na kwa nambari 7157, na 7175, na kwa nambari 7176, na 7177, na 7178, na 7179, na 7180. Na ameipokea Ibn Hibaan katika sahihi yake 3/215 kwa nambari 935, na 5/310, kwa nambari 1974, na Sha'iib Al-Arnautu alisema ni Hadithi nzuri (Hasan) katika "Sahih Ibn Hibaan", 5/312. Nao wahakiki wa "Musnad" walisema kwamba ni Hadithi nzuri (Hasan) kwa njia zake za upokezi, 28/338, na ameitaja Albaani katika "Silsilati Al-Ahaadithi Al-Sahihih" katika juzuu ya saba, kwa nambari 3228, na katika "Mawaarid Adh-Dhamaan" kwa nambari 2416, na 2418, na amesema: "Ni Hadithi sahihi kwa sababu ya upokezi mwingine."

126 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba Pepo ya Firdausi (ambayo) ndiyo Pepo ya juu zaidi."[88]

127 "Ewe Mwenyezi Mungu, ifanye upya imani ndani ya moyo wangu."[89]

128 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na swala isiyokuwa na manufaa."[90]

129 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na jirani mbaya, na mke atakayenitoa mvi kabla ya uzee, na kutokana na mtoto atakayekuwa bwana juu yangu, na kutokana na mali zitakazokuwa ni adhabu juu yangu, na kutokana na rafiki mwandani mwenye vitimbi, jicho lake likiniona na moyo wake ukinichunguza. Akiona jema, analifunika. Na akiona ovu, analitangaza."[91]



"Ewe Mwenyezi Mungu, usinipe hizaya siku ya Kiyama."[92]

130

88- Haya yamechukuliwa kutokana na kauli ya Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake -"... Kwa hivyo mnapomuomba Mwenyezi Mungu, basi muombeni Pepo ya Firdausi. Kwani hakika Pepo hiyo ndiyo Pepo ya kati na kati, na ndiyo Pepo ya juu zaidi, na juu yake ndiko kuna Kiti cha Enzi cha Mwenyezi Mungu, nako ndiko itokapo mito ya Pepo." Ameipokea Bukhari kwa nambari 2790, na nambari 7423.

89- Haya yamechukuliwa kutoka kwenye Hadithi ya Abdullahi Ibn Omari -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao - kwamba alisema: Amesema Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake -: "Hakika imani inazeeka ndani ya moyo wa mmoja wenu kama jinsi nguo inavyozeeka. Basi muombeni Mwenyezi Mungu azifanye upya imani ndani ya mioyo yenu." Ameipokea Al-Hakim 1/4, na akasema kwamba ni Hadithi sahihi na Adh-dhahabi akakubaliana naye. Na amesema Al-Haithami katika "Majma'i Az-Zawaaid" 1/52: "Ameipokea At-Tabaraani katika kitabu Al-Kabiir, na mtiririko wa mapokezi yake ni mzuri." Na Albaani alisema kwamba ni Hadithi nzuri katika "Silsilati Al-Ahaadithi As-Sahiiha", 4/113, kwa nambari 1585.

90- Abu Daud kwa nambari 1549, na akasema Albaani kwamba ni Hadithi sahihi katika Sahihi Sunan Abi Daud 1/424.

91- Ameipokea At-Tabaraani katika kitabu cha "Ad-Duaa", 3/1425 kwa nambari 1339, na akasema Albaani katika "Silsilat Al-Ahaadith As-Sahiiha", 7/377 kwa nambari 3137: "Nilisema: Na mtiririko huu wa upokezi ni mzuri, wapokezi wake wote ni wale wale wapokezi wa kitabu cha "At-Tahdhib..."

92- Ameipokea Ahmad katika "Musnad" 29/596, kwa nambari 18056, na wamesema wanaohakiki Musnad: "Mtiririko wa mapokezi yake ni sahihi". Na ameipokea At-Twabaraani katika "Al-Mu'ujam Al-Kabiir", 3/20, kwa nambari 2524 kwa matamshi haya: "Ewe Mwenyezi Mungu usinifedheheshe siku ya Kiyama, na wala usinifedheheshe siku yenye balaa."

131 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba salama Duniani na Akhera."[93]

132 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na elimu isiyofaa, na matendo yasiyopandishwa, na moyo usio na hofu, na kauli isiyosikika"[94]

133 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na msongo wa mawazo na huzuni, na kushindwa na uvivu, na ubahili na uoga, na uzito wa madeni, na kushindwa na watu."[95]

134 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na msongo wa mawazo na huzuni, na kushindwa na uvivu, na ubahili na uoga, na uzito wa madeni, na kushindwa na watu."[96]

135 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na adhabu ya Moto, na ninajikinga kwako kutoka na adhabu za kaburi, na ninajikinga kwako kutokana na majaribu yenye kuonekana na yasiyoonekana, na ninajikinga kwako kutokana na majaribu ya Masihi Dajjal"[97]

136 "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba kufa kwa ajili ya dini katika njia yako."[98]

93- Ameipokea Ahmad katika "Musnad" 29/596, kwa nambari 18056, na wamesema wanaohakiki Musnad: "Mtiririko wa mapokezi yake ni sahihi". Na ameipokea At-Twabaraani katika "Al-Mu'ujam Al-Kabiir", 3/20, kwa nambari 2524 kwa matamshi haya: "Ewe Mwenyezi Mungu usinifedheheshe siku ya Kiyama, na wala usinifedheheshe siku yenye balaa."

94- Ameipokea Ibn Maajah kwa nambari 3851, na amesema Albaani kwamba ni Hadithi sahihi katika Sahih Ibn Majah 3/259, na katika "Silsilat Al-Ahaadithi As-Sahiiha kwa nambari 1138.

95- Ameipokea Ibn Hibaan kwa nambari 2440 "Mawaarid" na amesema Albani kwamba ni Hadithi sahihi katika "Sahih Mawaarid Adh-Dhwamaan", 2/454, kwa nambari 2066.

96- Ameipokea Bukhari kwa nambari 6363. Alisema Anas, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: "Nilikuwa nikimtumikia Mtume wa Mwenyezi Mungu - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - kila mara anaposhuka mahali safarini, nilikuwa nikimsikia akisema mara nyingi: "Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninajikinga kwako..."

97- Ameipokea Muslim kwa nambari 2867, na ndani yake kuna: "Jilindeni kwa Mwenyezi Mungu kutokana na adhabu za Moto...", ["Jilindeni kwa Mwenyezi Mungu kutokana na adhabu za kaburi..."] mpaka mwisho wake.

98- Ameipokea Muslim kwa nambari 1909, na yaliyo kwenye mabano yanatokana na kauli yake Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-: "Atakayemuomba Mwenyezi Mungu kufa kwa ajili ya dini kwa ukweli, basi Mwenyezi Mungu atamfikisha daraja za waliokufa kwa ajili ya dini, hata kama atafia juu ya kitanda chake."



137 "Ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe. Ewe Mwenyezi Mungu, nifanye Siku ya Kiyama niwe juu ya wengi miongoni mwa viumbe wako katika watu. Ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe makosa yangu, na Siku ya Kiyama uniingize mahali patukufu pa kuingia."[99]

138 "Ewe Mwenyezi Mungu, niongoe miongoni mwa uliowaongoa, na unipe salama miongoni mwa waliopewa salama, na unisimamie miongoni mwa uliowasimamia, na unibariki katika kile ulichonipa, na unikinge kutokana na shari ulizozipitisha, kwani hatodhalilika uliyemuweka karibu, umetukuka Mola wetu Mlezi na umetakasika."[100]

139 "Mola wangu Mlezi, nisamehe makosa yangu siku ya Malipo."[101]

140 "Ninaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu Mkuu, ambaye hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki ila Yeye, aliye Hai, Mwenye kusimamia mambo yote milele, na ninatubia kwake."[102]

99- Ameipokea Bukhari kwa nambari 4323, na Muslim kwa nambari 2498, nayo imechukuliwa kutoka kwenye maombi ya Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - alipomuombea 'Ubeid Abi 'Amir, na kutokana na maombi yake - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - alipomuombea Abuu Burdah, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao.

100- Ameipokea Ahmad katika "Musnad" 3/249 kwa nambari 1723, na wamesema wahakiki wa "Musnad" 3/249: "Mtiririko wa mapokezi yake ni sahihi." Na upokezi huu ni wa moja kwa moja bila kuifungamanisha na swala ya witri kama jinsi ilivyokuja katika mapokezi mengine. Katika upokezi huu, alisema Anas, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, "Alikuwa Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, akitufundisha maombi haya..."

101- Ameipokea Muslim kwa nambari 214. Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, aliambiwa: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika Ibn Jud'aan alikuwa katika zama za ujinga akiunganisha udugu, na akiwalisha masikini. Je, hayo yatamnufaisha? Akasema: "Hayatamsaidia. Hakika yeye hakusema hata siku moja Mola wangu Mlezi nisamehe makosa yangu Siku ya Malipo."

102- Ameipokea At-Tirmidhi kwa nambari 3577, na Albani akasema kwamba ni hadithi sahihi katika Sahih At-Tirmidhi 3/469: "Atakayeyasema maneno haya, Mwenyezi Mungu atamsamehe hata kama alikimbia kutoka katika safu za vita vya kidini."

141 "Ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe makosa yangu, na niondoshee chuki ndani ya moyo wangu, na unikinge kutokana na majaribu yenye kupotosha."[103]

142 "Ewe Mwenyezi Mungu, nibakishe hai kwenye mwenendo wa Nabii wako - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - na unifishe nikiwa kwenye mila yake, na unikinge kutokana na majaribu yenye kupotosha."[104]



103- Haya yamechukuliwa kutoka katika maombi ya Mtume -rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - alipomuombea Aisha - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: "Ewe Mwenyezi Mungu, msamehe makosa yake, na muondoshee chuki ndani ya moyo wake, na mkinge kutokana na majaribu yenye kupotosha." Ameipokea Ibn Asaakir kwa mapokezi yake katika "Al-Arbauna fii manaaqib ummahaat Al-Muuminina" ukurasa wa 85 kutoka kwa Aisha, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na alisema: "Hadithi hii ni sahihi nzuri (Sahiihun Hasan), kutokana na hadithi ya Baqiyah Ibn Al-Waliid." Na ameipokea Ibn As-Suniyyi kwa mfano wake katika 'A'amalu Al-Yaumi wallailah, kwa nambari 457, na katika nakala nyingine ya Ibn Suniyyi alisema: "Na unikinge kutokana na Shetani" badala ya "kutokana na majaribu yenye kupotosha." Angalia upokezi wake kwa Albaani katika kitabu "Adh-Dhaifu" kwa nambari 4207. Hadithi hii inatiliwa nguvu na hadithi zingine kutoka kwa Ummu Salamah - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - na inapatikana kwa Ahmad kwa nambari 26576, 44/2 kwa mfano wake, na matamshi yake ni: "Sema: 'Ewe Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa Nabii Muhammad, nisamehe makosa yangu, na uniondoshee chuki ndani ya moyo wangu, na unikinge kutokana na majaribu yenye kupotosha kwa muda wote utakaotuweka hai." Al-Haithami alisema kwamba ni Hadithi nzuri katika "Majmau' Az-Zawaaid" 10/27. Vile vile, ipo kwa At-Twabaraani katika "Al-Muujam Al-Kabiir" 23/388 kwa nambari 785 bila ya matamshi yake: "Kwa muda wote utakaotuweka hai." Na hadithi hii ina ushahidi kutokana na Hadithi ya Ummu Haanii -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - kwamba alisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, nifundishe maombi nitakayokuwa nikiomba, akasema: "Sema: 'Ewe Mwenyezi Mungu, nisamehe makosa yangu...'" Hadithi hii ameipokea Al-Kharaaitwii katika kitabu "Al-i'itilaal Al-Quluub" kwa nambari 52, na katika "Masaawi'u Al-Akhlaaq" kwa nambari 323.

104- Ameipokea Al-Baihaq katika Al-Kubraa, 5/95 kutokana na maombi ya Ibn Omari ikiwa ni maombi yaliyosimamia kwake, na amenukuu hayo Ibn Al-Mulaqqin katika kitabu "Al-Badri Al-Muniir" 6/309, na amesema hali ya kunukuu kutoka katika kitabu "Adh- Dhwiyaai": "Mapokezi yake ni mazuri" na amesema Ibn Masud - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: "Asiseme mmoja wenu: Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na majaribu, kwani hakuna yeyote isipokuwa anakuwa amefungamana na majaribu. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu anasema: "Hakika ya mali zenu na watoto wenu ni majaribu." (Surah Taghabun:15) Basi yeyote atakayejikinga, basi ajikinge kwa Mwenyezi Mungu kutokana na majaribu yenye kupotosha. Ameipokea Ibn Jarir, katika Tafsiri yake,13/475 kwa namabri 15912, na ameitaja Ibn Batwaal katika ufafanuzi wake wa Sahihi Al-Bukhari, 4/13.

143

"Ewe Mwenyezi Mungu, shusha rehema juu ya Muhammad na wafuasi wake Muhammad kama ulivyoshusha rehema juu ya Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim. Hakika Wewe ni Msifiwa, Mtukufu. Na shusha baraka juu ya Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama ulivyoshusha baraka juu ya Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim. Hakika Wewe ewe ni Msifiwa, Mtukufu."[105]

Na kila sifa njema ni zake Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe wote, kama inavyoendana na utukufu wake, na ukubwa wa utawala wake. Ewe Mwenyezi Mungu, teremsha rehema na amani juu ya Nabii wetu Muhammad na juu ya watu wake, na Maswahaba zake, na waliomfuata kwa wema mpaka siku ya Malipo.

105- Ameipokea Bukhari kwa nambari 3370, na yaliyo baina ya mabano yanayotokana na Hadithi ya Abuu Huraira - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - yanapatikana kwa Muslim kwa nambari 405.

تعرف على الإسلام

بأكثر من 100 لغة

موسوعة القرآن الكريم
QuranEnc.com

ترجمات متقنة لمعاني القرآن الكريم بأكثر من (75) لغة

بيان الإسلام
byenah.com

مواد منتقاة للتعريف بالإسلام وتعليمه بأكثر من (120) لغة

موسوعة الأحاديث النبوية
HadeethEnc.com

ترجمات متقنة للأحاديث النبوية وشروحها بأكثر من (60) لغة

ضيوف الرحمن
hajjumrh.com

مواد منتقاة للحجـــاج والمعتمرين و الزوار بلغات العالم

جامع المحتوى الإسلامي باللغات
islamcontent.com

مواد إسلامية متنوعة وشاملة بأكثر من (125) لغة

موسوعات وخدمات إسلامية باللغات
s.islamenc.com

للمزيد من المواقع الإسلامية بلغـــات العـــالم

ضيوف الرحمن
hajjumrh.com

جمعية خدمة المحتوى الإسلامي باللغات